

# Pambazuko

Toleo Namba 056

Jumatatu Januari 8-14, 2024

**Mbowe  
aunganisha  
taifa  
kupitia  
kanisa**

**Uk. 7**



**Tanzania  
yapiku  
Kenya  
kukua  
uchumi**

**Uk. 8**



**Jicho la Tai**

**'Napambana  
na Samia  
urais  
2025'**

**Uk. 5**



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

## Imani 10 za waandishi wa Pambazuko

**G**AZETI la Pambazuko linandelea kujenga heshima kwa kuwapa wasomaji wake habari ambazo zimefanyiwa kazi kwa kina.

Pambazuko, likiwa linakaribia kufikia umri wa miaka miwili, limekuwa gazeti la mfano na rejea mahali pengi tangu kianzishwa kwake mwaka juzi na linaendelea kujiimarisha kitaaluma kadri inavyowezekana.

Ni kutokana na imani kutoka kwa wasomaji wake, tumeona ni vyema kuweka kwa umma misingi na imani za waandishi wa habari wa Pambazuko ili kila msomaji atambue kuwa watendaji wa Pambazuko wanasimama katika imani za namna gani.

Watu wengi wameuliza, je, Pambazuko ni gazeti kama magazeti mengine, mbona limekaa tofauti na watendaji wa vyombo vingine vya habari ambavyo vimezoeleka?

Jibu la swali hili ni rahisi kwa maana kwamba waandishi wa habari wa Pambazuko wanasimamia imani 10 ambazo zimekuwa mwongozo wa utendaji wao wa kila siku.

Pamoja na kwamba gazeti hili husambazwa bure kwa njia ya WhasApp, email na Telegram, ni chombo ambacho kimesajiliwa na kutambuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pande zote mbili; Tanzania Bara na Zanzibar.

Hivyo, ni chombo cha habari chenye hadhi sawa na magazeti, redio, vituo vya televisheni na vyombo vingine rasmi na vinavyotambuliika.

Imani 10 za mwandishi wa Pambazuko

1. Kwamba kufikiri na kuamua kwa uwazi, usahihi na kuandika habari

kwa kuzingatia miiko ya uandishi wa habari ndiyo msingi wa kazi zangu.

2. Kwamba kamwe sitaandika habari za kutunga, uongo wala uzandiki kwa lengo la kudanganya jamii au kuumiza yeyote.

3. Kwamba nitahakikisha kinachopeleka kwa mhariri ni ukweli, tena ukweli mtupu.

4. Kwamba nitaweza kuitetea – kwa ushahidi, habari ambayo nitaandika hata ikiwa ni mahakamiani.

5. Kwamba nitashiriki kuhakikisha matangazo, habari, makala, safu na hata barua za wasomaji zinazingatia miiko ya uandishi wa habari na kamwe hazina lengo lililojificha.

6. Kwamba ubora wa kazi zangu – kupitia Pambazuko, utapimwa kwa uadilifu, uaminifu na usahihi wa kile kinachochapisha.

7. Kwamba, kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa na uandishi bora, elimu bora; darasani na chumba cha habari cha Pambazuko, ni sehemu muhimu kujiendeleza kitaaluma.

8. Kwamba sitaogopa kuandika ukweli, hata kama utaumiza baadhi ya watu. Lengo ni kuponya jamii pana.

9. Kwamba rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea na nitaandika wanaojihusisha nayo ili kuokoa jamii.

10. Ninaamini kuwa uandishi bora wa habari siku zote unajali utu, kamwe sitabagua.

Imani hizi ndiyo msingi wa kutenda kazi ndani ya chumba cha habari cha Pambazuko tangu kuanzishwa kwake na kwamba zitasimamiwa kwa wivu mkubwa katika kulinda heshima, taaluma na utu.

Mhariri Mkuu  
Januari 07, 2024

## WATANZANIA WEMA SANA...



*Mchezaji mahiri wa zamani wa Yanga na Simba, Bernard Morrison (Tototundu), akiwa nyumbani kwake Takoradi, Ghana, juzi amekutana na Nick Reynolds (Bongo Zozo) na kutamka kwamba "Watanzania ni watu wema sana." Huku akisema anapenda kupata uraia wa Tanzania. (Picha kutoka Instagram ya Bongo Zozo).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### NUKUU



*MUNGU alitumia hekima kubwa mno kufanya binadamu tusijuane mioyoni mwa mwingine anawaza nini juu yako, pia tuisomane mawazo ya kila mmoja wetu; vinginevyo kusingekuwa na udugu, urafiki, wala ujirani - Dina Marios, mtangazaji wa Radio EFM.*

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



## **Napambana na Samia urais 2025**

Na Igo AI

**M**OJA ya maazimio ya komredi Tai - kwa mwaka huu, 2024 ni “kujifua” kwa ajili ya kugombea nafasi kubwa ya kisiasa mwakani, 2025.

Nafasi hiyo ni urais; kwamba anatamani kuwa kiongozi mkuu wa Tanzania na watu wake; lije jua, inye mvua. Lazima akomae na ahakikishe anupata.

Hata hivyo, Tai hakutaka kuweka hadharani mipango aliyoinuia, achilia mbali maazimio yake kwa mwaka huu mpya, lakini amesukumwa na kauli za baadhi ya viongozi wa serikali ya sasa na wale wa chama tawala; Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Sababu za kugoma kuweka maazimio yake hadharani, ni woga wake wa kufanyiwa fitna, dhihaka na hata anda na watu ambao anawafahamu vilivyo; kwamba wengi wamejaa roho mbaya na wanafanya hivyo bila sababu za msingi.

Lakini, Tai alivyosikia kauli ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuonekana kuungwa mkono na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Komredi mwenzake, Alhaj Abdulrahman Kinana, akaona asikae kimya; lolote linaweza kutokea na ndoto yake kukatizwa.

Akiwa amejipumzisha mahala, Tai aliwasikia vigogo hao wakisema kwamba wanafikiri kujiandaa kuvishawishi, ingawa wataviambia tu - vikao vya wakubwa ndani ya chama chao, eti mwenyekiti wao, Rais Samia Suluhu Hassan awe mgombea pekee wa nafasi ya urais wa nchi yetu.

Eti wakubwa hao watakusanya nguvu za kuhakikisha kuwa fomu itakayotolewa ya kugombea nafasi ya urais iwe moja tu.

Kwamba mitambo mikubwa ya kuchapisha fomu za wagombea iwashwe; utumike umeme; walipwe watendaji; zinunuliwe karatasi, halafu ichapwe fomu moja tu.



*Rais Samia Suluhu Hassan*

Tai kusikia hivyo, akaona haiwezekani, akamuita mwandishi wake, huku akionekana kufura na kukasirishwa na kauli za makomredi wenzake.

“Hivi hawa watu wana akili gani, nani kawatuma, mbona wanataka kugeuza chama chetu kuwa cha kidikteta, nani kawaambia mama anaogopa ushindani,” akang’aka Tai.

Hakukoma hapo, akaendelea; “yaani mambo mazuri yanayofanywa na mama yetu, leo wanajidai kumkingia kifua eti asipate ushindani ndani ya chama chetu, hawa watu ni shida sana,” Tai akatoa maneno makali mengine ambayo mwandishi wake ameyachuja.

Ohh! Tai akaonekana akibubujikwa chozi, akidai kwamba ni vyema mama akaachwa apambane ndani ya chama chao, ili kujua atapata nini kwenye boksi la kura wakienda kwa wananchi?

Tai anaona kuchapisha fomu moja ya mgombea ni fitna kwake na kwamba ni kuitukanisha demokrasia.

Hivyo, sasa naye ameamua kuchukua ‘maokoto’ yake, kuingia kwa kila mjumbe wa vikao vya chama chao ili kuwashawishi wakatae kuchapishwa fomu moja, na ameapa kwamba atashawishi kwa njia mbili kubwa ambazo zimezoeleka; maneno matamu na “kuweka grisi” kwa kila mmoja. Hataki mchezo kabisa Tai.

•**Ukipenda kuwasiliana na Tai, tumia namba ya mwandishi wake; 0754 020 880**

## Habari

## Mbowe aunganisha taifa kupitia kanisa

Na Scovya MANASE

**M**WENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ametenda wanayopaswa kufanya wanasiasa wa Tanzania; ameunganisha taifa kupitia Kanisa.

Kwamba Mbowe hakujali itikadi za kisiasa, dini, madhehebu, wala mipaka; alishawishi Watanzania kuchangia huduma ya kusambaza na kuhubiri amani, neema, heri na utangamano wa Tanzania.

Siku ya mwisho ya mwaka jana, 2023 itabaki kuwa kumbukumbu nzuri kwa wapenda amani Tanzania, kwani wanasiasa waliweka tofauti zao na kuungana mkono changisho la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Tanzania (KKKT)-Bathel, Usharika wa Nshara, Machame, Kilimanjaro.

Jumla ya Shilingi milioni 887 zilichangwa na wale walioitwa “marafiki wa Mbowe,” akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan aliyechangia Shilingi milioni 150.

Katika Ibada ya Jumapili hiyo ya mwisho ya mwaka jana, 2023, Mbowe aliungana na wanasiasa wengine wakiwamo Halima Mdee, Ester Bulaya, Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, mawaziri, wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wengine wa serikali.

Hata hivyo, ushawishi wa Mbowe “kuwavuta” hata wapinzani wake kisiasa, kuchangia, kulizua gumzo kwenye viunga vya mitandao ya kijamii; wakiwamo wanaomshutumu na wengine kumuunga mkono.

Wapo wanaodai kwamba hatua ya Mbowe ndiyo inapaswa kufuatwa na wanasiasa wa Tanzania; kwa maana ya kwamba kamwe siasa siyo uadui.

Kwamba alichokifanya Mbowe ni kuweka siasa pembeni na kusukumwa na dhamira njema ya kuchangia kazi za Mungu; ambaye hana ubaguzi na



*Askofu Dkt. Frederick Shoo aliongoza harambee*

haangalii itikadi wala rangi za watu anapotenda kazi zake.

Wapo pia wanaodai kwamba Mbowe kutangaza kwamba amechangiwa na Rais Samia Shilingi milioni 150, ni kumjenga “mpinzani” wake, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Tanzania mwaka kesho, 2025.

Hata hivyo, wanazuoni na wachambuzi makini wa masuala ya siasa wanadai kuwa Mbowe ndiye amejijenga zaidi badala ya “kujimaliza,” kwani ndiye amewafikia wale wapinzani wake na kukubali “kumshika mkono” kuinua Kazi za Mungu.

“Lengo la harambee kamwe haikuwa kuinufasisha Chadema wala haikuwa lengo kumfifisha Rais Samia; lengo kubwa lilikuwa kuchangia maendeleo ya kanisa na kumpa Mungu utukufu, na zaidi sana kuchochea huduma bora kwa wananchi,” amesema Maalim Hamis Kamelya wa Kituo cha Kukuza Elimu, Dar es Salaam.

Dkt. Willbroad Slaa, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chadema, alisema angependa kuona Rais Samia anapeleka fedha hizo kanisani kwa kupitia kwa viongozi wa serikali, badala ya kumpa Mbowe. Hata hivyo, Slaa hakufanua zaidi.



**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## Mezani kwa Chahali

### 2024: Changamoto zaidi kuonekana

**N**IANZE makala haya kwa kuomba radhi kutokana na ukimya wa muda mrefu uliojitokeza, baada ya safu hii kusimama. Hali hiyo ilisababishwa na sababu nje ya uwezo wangu.

Hata hivyo, safu hii inarejea ikiwa na utofauti kidogo, ambapo badala ya mada za siasa, hususan za Tanzania, sasa itajikita zaidi katika masuala ya kimataifa.

Haimaanishi kuwa safu haitogusa kabisa masuala ya Tanzania, bali kipaumbele zaidi kitakuwa kwenye masuala ya kimataifa.

Makala haya ya kwanza yanatupia jicho changamoto za mwaka 2024 kwa muktadha wa masuala makubwa katika mwaka 2023, nchini Tanzania, barani Afrika, na duniani kwa ujumla.

Kwa Tanzania, yayumkinika kutanabaisha kuwa changamoto kubwa zaidi katika mwaka 2023 ilikuwa ufisadi. Na moja ya athari kubwa zaidi za ufisadi huo ni kwenye sekta mbalimbali za kimbakati, ikiwamo nishati.

Ndio maana mara nyingi tu, sababu zinazotolewa na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco) kuhusu mgao wa nishati hiyo hakika kwangu hazina mashiko.

Kwa mfano, “kupungua kwa kina cha maji kwenye vyanzo vya kuzalisha umeme -” hata kukiwa na mvua kubwa za kusababisha mafuriko, bado tatizo la mgao lipo palepale.

Tatizo hili la umeme litaendelea pia mwaka 2024, na njia pekee ya kumaliza tatizo hilo ni kupambana na chanzo – na siyo athari. Na chanzo ni kuwepo kwa mambo yanayofanywa na baadhi ya viongozi wa Tanesco na wale wa serikali kufanya hujuma.

Kibaya zaidi, wakubwa hao wanaendelea kufanya mambo hayo ya hovyo, huku Taasisi ya Kuzuia na



Kupambana na Rushwa (Takukuru) ikiangalia tu.

Kila mara utasikia viongozi wakitoka maagizo kwa taasisi hiyo ichukue hatua, lakini hakuna kinachofanyika.

Mbali na hilo jambo sugu kwa Tanesco, tuangalie changamoto kadhaa za kiusalama mwaka 2023 – katika Afrika, hususan janga la ugaidi katika Ukanda wa Sahel. H

Huko kunatarajiwa kuendelea kuwepo matishio ya usalama katika nchi za Niger, Mali, Burkina Faso, Guinea na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Kadhalika, hali ya usalama huko Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Sudan na Libya itaendelea kuwa tete.

Nje ya Afrika, vita ya Gaza inatarajiwa kupanuka zaidi hadi Israeli itapoamua suluhisho la kidiplomasia badala ya kijeshi.

Kwa upande mwingine, vita ya Ukraine dhidi ya Russia, inaweza kumalizika mwaka huu. Tayari kuna tetesi kuwa Marekani na Ujerumani zinaandaa mpango wa kuishinikiza Ukraine ikubali baadhi ya matakwa ya Urusi, kutokana na “wafadhili” hao wa Ukraine kuelemeza na gharama za kuisaidia nchi hiyo.

Heri wa mwaka mpya, 2024

•Tafadhali nifuatilie hapa: [https://instagram.com/evarist\\_chahali](https://instagram.com/evarist_chahali)

## Habari

## Tanzania yapiku Kenya kukua uchumi

Na Peter ANDREA

**T**ANZANIA imeshika nafasi ya 15 kati ya nchi 20 bora duniani kwa kuzingatia matokeo ya kasi ya ukuaji wa pato la taifa katika mwaka 2024.

Nchi hiyo ya Afrika Mashariki inaelezwa na wabobezi wa uchumi wa dunia kuwa pato lake linakua kwa kasi ya asilimia 6.1 kwa mwaka.

Hivyo, Tanzania inashika nafasi ya 10 ndani ya nchi za Afrika, nafasi ya pili ndani ya nchi za Afrika Mashariki, ikitanguliwa na Rwanda, wakati Kenya na Uganda ziko nje ya nchi 20 bora duniani.

Mataifa haya 20, asilimia za kasi ya ukuaji wa uchumi wake zikiwa kwenye mabano ni kama ifuatavyo: Macao (27.2), Guyana (26.6), Palau (12.4), Niger (11.1), Senegal (8.8), Libya (7.5), Rwanda (7.0), Ivory Coast (6.6), Burkina Faso (6.4), Benin (6.3), India (6.3), The Gambia (6.2), Ethiopia (6.2), Cambodia (6.1), Tanzania (6.1), Bangladesh (6.0), Djibouti (6.0), Burundi (6.0), Philippines (5.9), na Vietnam (5.8).

Wastani wa kasi ya ukuaji wa pato la dunia ni asilimia 2.9.

Takwimu hizi ni kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi duniani iliyoandaliwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na kutundikwa kwenye tovuti yake rasmi Oktoba 2023.

Taarifa hii inaonesha kuwa katika ngazi ya ulimwengu, Macau, eneo maalum la utawala la China, linaongoza kwa makadirio ya ukuaji wa asilimia 27 ikifuatiwa na Guyana kwa asilimia 26.

Kulingana na ripoti ya IMF, makadirio



Wasiri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba

ya ukuaji wa uchumi duniani kwa mwaka ujao ni asilimia 2.9 tu, chini sana ya makadirio ya nchi nyingi za Afrika.

“Kwa kifupi, tunaweza kuona kwa urahisi kwamba Barani la Afrika linayo kesho njema”, ripoti hiyo inasema.

Kwa mujibu wa taarifa hii ya IMF, nchi nyingi zinazotarajiwa kupata kasi kubwa ya uchumi ziko barani Afrika na Asia, ambapo asilimia 60 zinatoka Afrika, kwa pamoja zikiwa na wastani wa kasi ya ukuaji wa pato la taifa la asilimia 7.02.

Nchi saba za Bara la Asia, ambazo ni asilimia 35 ya mataifa haya 20 yaliyo bora, zina wastani wa kasi ya ukuaji wa pato la taifa la asilimia 9.96. Nchi pekee ya Amerika iliyo katika nchi 20 bora ni Guyana yenye kasi ya ukuaji wa pato la taifa ya asilimia 26.6.

Ni nchi tatu pekee za Afrika Mashariki zimefanikiwa kuingia katika orodha hii ya mataifa 20 bora duniani, zote kwa pamoja zikiwa na wastani wa kasi ya ukuaji wa pato la Taifa ya asilimia 6.37, Rwanda ikiwa na asilimia saba, Tanzania asilia 6.1 na Burundi asilimia 6.0.

## Mbowe aunganisha taifa kupitia kanisa

Inatoka Uk. 6

Askofu Dkt. Benson Bagonza ameonsha kushangaza na wanaolalamika Mbowe kukusanya fedha kutoka kwa Rais Samia kwa kuwa yeye

ameshawishi, amepewa fedha, amepeleka kanisani, sasa hapo nani mwenye kubeba sifa ndani ya kanisa na hata nje.

Dkt. Bagonza anahoji, je, anayepata sifa hapa ni aliyeshawishi fedha ikatolewa ama aliyetoa?





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Viongozi wetu wasitumie ubabe kuamua

**W**ABOBEZI wanafasiri kwamba sheria ni mfumo wa kanuni na taratibu zilizowekwa kwenye jamii na mamlaka kwa ajili ya kuongoza matendo yao na uhusiano wao.

Sheria pia ina maana ya utaratibu unaotengeneza mfumo na mwelekeo wa maisha chini ya mamlaka husika.

Kifupi, tunaweza kusema kuwa, sheria ni msingi wa uhai wa jamii yoyote ile; iwe kubwa au ndogo, zote zinahitaji uwepo wa sheria, maana pasipo na sheria, kila mmoja atafanya atakayo na kukosekana amani na uthabiti kwa maisha ya watu.

Tukio la Desemba 13, 2023 la wanamgambo wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, mkoani Rukwa kufyeka heka mbili za mahindi yaliyolimwa karibu na makazi ya watu kufuatia agizo linalokataza kulima mazao hayo, haliwezi kuachwa bila kujadiliwa.

Sina shida yoyote na uamuzi huu wa kikatili kwa sababu wanamgambo hao walikuwa wakitekeleza amri 'halali' ya mkurugenzi wa halmashauri ya manispaa hiyo, Sophia Kumbuli aliyotoa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji ya Halmashauri namba 355 chini ya kanuni kifungu namba 77(1) (r) namba (5).

Nimesema hapo juu kwamba sina shaka kwa kuwa naelewa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imetoa nafasi ya kuundwa kwa sheria ndogondogo kwa ajili ya kuongoza jamii. Na Halmashauri ya Mpanda iko sahihi kutunga na kutekeleza sheria hiyo.

Na yeyote yule hawezi kuwalaumu kwa uamuzi ule wa kufyeka hekari mbili za chakula kilichobakiza siku chache kukomaa, licha ya kutafsiriwa kukosa ubinadamu kwa kuwa, sheria ya ardhi iliyotungwa na bunge imegawanya matumizi kati ya mijini na vijijini.

Na ukiisoma vizuri sheria ya matumizi



*Mahindi yaliyofyeka kwa mbali na serikali huko Mpanda- Picha ya Mwananchi*

ya ardhi, mijini hakutakiwi hata kufugwa kuku wala kulima mazao yoyote kama yale mahindi "yaliyofyeka kwa mbali" huko Mpanda!

Sawa, mkulima huyo amefanya kosa la kukiuka sheria na kanuni za halmashauri ya manispaa hiyo, na hata pengine sheria ya mazingira, lakini najuiliza mpaka mazao hayo yamefikia hatua ya kukaribia kukomaa viongozi wa Mpanda walikuwa wapi?

Pamoja na kufuata sheria, viongozi wetu wa Mpanda hawaoni kufyeka mahindi hekari mbili yaliyosalia siku chache kukomaa, kunaaweza kumgombanisha Rais Samia Suluhu Hassan na wananchi wake, akaonekana hana huruma?

Tuseme waheshimiwa viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda walishindwa nini kwenda mapema kumuamrisha ayang'oe walau akawauzie wafugaji wafanye malisho ya wanyama wao?

Hakika kilichofanywa na wakubwa hao, pamoja na kuwepo sheria, walipaswa kuzukumwa na utu, Utanzania na zaidi sana, ubinadamu.

*Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu namba 0784 43 85 46*

*Barua pepe; mtagaluka@gmail.com*

**Habari****Tishio jipya la kuibuka Covid-19**

Na Tryruckia MFINANGA

**O**NGEZEKO la changamoto ya magonjwa ya mfumo wa hewa, kwa nchi nyingi za Afrika, Tanzania ikiwamo, limeshtusha Shirika la Afya Duniani (WHO) kutoa hadhari.

Adhari iliyotolewa na WHO jana imewataka watu wote kuwa makini na kuchukua hatua za kukabili hali hiyo ambayo inafananishwa na dalili za Covid-19.

WHO inaeleza kwamba changamoto hiyo ya mfumo wa upumuaji inakuja ikiwa na dalili za joto la mwili la mtu upanda kuliko kawaida, mafua na kukosa hamu ya kula.

Pia changamoto hiyo inakuja na vimelea vingine vya magonjwa ya mfumo huo, huku shirika hilo likieleza kuwepo kwa dalili za kuongezeka, hasa kwenye nchi zenye joto.

“Ni vyema watu wakarejea utaratibu wa kupima kutambua kama wameambukizwa Covid 19 na huduma huyo waipate kutoka kwa wataalamu afya wenye kuthibitishwa na serikali,” anasema Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dkt. Tedros Adhanom.

“Endelea kutumia barakoa, hakikisha hewa safi ya kutosha mahali ulipo na uhakikishe kuwa wewe na wapendwa wako mmempata chanjo zinazohitajika za Covid-19,” anaongeza daktari huyo.

Wataalamu wa afya wanasema takriban nusu ya waathiriwa wa Covid 19 katika nchi za Afrika wanaripoti angalau dalili moja kati ya nyingi zinazoweza kuwa za Covid 19 na hali hiyo kuendelea kwa siku kadhaa.

Watafiti wanasema uchovu na dalili zingine zinazoendelea tayari zinaathiri ubora wa maisha ya watu na zinaweza kudhoofisha uwezo wao wa kufanya kazi, na kuwafanya wawe katika hatari kupata maambukizi mapya kwa urahisi.

Ingawa siyo tishio la kimataifa tena,



**Waziri wa Afya - Ummy Mwalimu**

bado Covid 19 inaendelea kuripotiwa katika sehemu tofauti Afrika.

Kulingana na vituo vya kudhibiti magonjwa Afrika, Africa CDC, tangu janga la Covid - 19 kuanza 2019, imethibitika kesi zaidi ya 12,216,748 zimeripotiwa barani Afrika hadi sasa.

**Eneo la Kusini mwa Afrika**

WHO bado inasaidia serikali kupata uwezo wa kufanya vipimo vya tishio la afya linaloambatana na changamoto ya mfumo wa kupumua.

“ Serikali zinafaa kuhakikisha wananchi wanapata vipimo vya kuaminika, matibabu na chanjo, haswa kwa wale ambao wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa,” anaongezea Adhanom.

Mwaka huu, Rwanda imeanza kujitayarisha kuzalisha chanjo aina tofauti ikiwemo chanjo dhidi ya Covid 19. Kampuni ya kuzalisha dawa za chanjo ya Ujerumani, BioNTech imefungua kiwanda chake Jijini Kigali, Rwanda.

Kiwanda hicho kimeanzishwa kwa ajili ya kutengeneza chanjo ili kusaidia upatikanaji wake kwa nchi za Afrika.

Rwanda sasa itaweza kutoa hadi dozi milioni 50 za bidhaa kila mwaka na kuifanya kuwa nchi ya kwanza Afrika kuwa na kiwanda kikubwa cha kuzalisha bidhaa hiyo na zingine ambazo zitasaidia kuharakisha upatikanaji wake.

# Ukiwa Bukoba...

## Furahia *Nowe* Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya:

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

**Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.**

**Wasiliana nasi kwa namba hii:**

**\*0753949488\***



## Mapitio ya Kitabu

### Ujasusi: Ni nini?

Na Mwandishi WETU

**K**ITABU hiki chenye kurasa 191 kimeandikwa na kuchapishwa na Mtanzania mwenye makazi yake nchini Uingereza, Evarist Chahali,

Mwandishi huyo amechapisha vitabu 16, lakini ni viwili tu ambavyo vipo katika nakala dhahiri (hard copies); Ujasusi kilichochapishwa Novemba, 2023 na kingine Afisa Usalama wa Taifa Ni Mtu wa Aina Gani? Na Anafanya Nini? Kikifahamika zaidi kwa jina la Kitabu cha Shushushu, kilichochapishwa mwaka 2016.

Ingawa vitabu hivyo viwili vyote vinahusu taaluma ya intelijensia, vina tofauti moja ya msingi. Wakati kitabu cha “shushushu” kinahusu taaluma ya “Uafisa Usalama wa Taifa” kwa ujumla, kitabu cha Ujasusi kinahusu moja ya maeneo manne makuu ndani ya taaluma ya intelijensia, yaani ujasusi, ugaidi, uzandiki na hujuma.

Kwa pamoja maeneo hayo hujulikana kiintelijensia kama “shughuli za adui” (enemy activities).

Ni hivi, jukumu kuu kwa taasisi za intelijensia duniani ni kuzuia hizo “shughuli za adui,” lakini ili ziweze kufanikisha hilo, nazo zinalazimika kufanya hizo “shughuli za adui” japo siyo wakati wote, na siyo zote.

Kitabu cha “Ujasusi Ni Nini? Na Je Majasusi Wanafanya Kazi Gani Hasa?” kina sura 19, kama ifuatavyo.

Sura ya kwanza: Maana ya UJASUSI

Sura ya pili: Historia ya Ujasusi

Sura ya tatu: Aina za Ujasusi


Sura ya nne: Ujasusi wa Kimtandao (Cyberespionage) ni Nini?

Sura ya tano: Ujasusi kama nyenzo ya diplomasia

Sura ya sita: Ujasusi unavyotumika kidiplomasia

Sura ya saba: Kifuniko (cover) cha jasusi

Sura ya nane: Tofauti kati ya



jasusi (spy) na afisa usalama wa taifa (Intelligence Officer)

Sura ya tisa: Mtu anawezaje kuwa jasusi? (majasusi wanapatikanaje?).

Sura ya kumi: Jinsi jasusi anavyopata watoa habari nje ya nchi na kujipenyeza eneo kusudiwa.

Sura ya kumi na moja: Majasusi kazini.

Sura ya kumi na mbili: Majasusi kazini - roho mkononi.

Sura ya kumi na tatu: Kufuatiliwa (Surveillance).

Sura ya kumi na nne: Jinsi jasusi anavyowakwepa wanaomfuatilia (Counter-Surveillance).

Sura ya kumi na tano: Ngoni kama nyenzo ya ujasusi (sexespionage).

Sura ya kumi na sita: Maneno/lugha ya kijasusi.

Sura ya kumi na saba: Changamoto zinazokabili ujasusi/majasusi duniani.

Sura ya kumi na nane: Changamoto zinazokabili ujasusi/majasusi Tanzania.

Sura ya kumi na tisa: Mashirika maarufu ya ujasusi duniani na majasusi maarufu duniani.

Kitabu kinauzwa shilingi 45,000 na kinafikishwa kwa mnunuzi bure popote alipo kwa Jiji la Dar es Salaam. Wateja wa mikoani watapokea nakala ya kitabu kwa kuongeza fedha za usafirishaji shilingi 5,000 tu.

**Tafadhali nunua nakala ya kitabu hicho kupitia M-Pesa 0767-340-975 na jina litakaloonekana ni ANNA.**

100% TRUSTED BRAND



# **DOR** **EASY WASH**

**LIQUID SOAPS**

**USAFI WAKO  
NI JUKUMU LETU**

MANUFACTURED BY: DOR EASY WASH  
P.O BOX 80159 KIBADA, KIGAMBONI | DAR ES SALAAM - TANZANIA  
MOB: +255 715 771 123 | EMAIL: DOREASYWASH@GMAIL.COM

## Tangazo



# Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au

Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Burundi yaonya Rwanda kusaidia waasi

Na Mwandishi WETU

**S**ERIKALI ya Rwanda imekanusha vikali kauli ya Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye kwamba inasaidia kuchechea maasi ndani ya nchi yake.

Rais Ndayishimiye ameituhumu Rwanda kwamba imekuwa ikifadhili makundi ya waasi wenye silaha za kivita wa Burundi ambayo yameweka kambi mashariki wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Msemaji wa Serikali ya Rwanda, Yolande Makolo, amekanusha madai hayo na kudai kuwa “hayana msingi” na kwamba yanabebwa na hisia zaidi.

“Hakuna ukweli katika maoni ya Rais wa Burundi kuhusu Rwanda,” Makolo alijibu kwenye mtandao wa X (zamani Twitter) Ijumaa iliyopita.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara katika mji wa Cankuzo, Rais Ndayishimiye aliishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa Red-Tabara, kwamba linasaidiwa na Rwanda.

“Hawa waasi wamepeva nyumba, wanawezeshwa fedha na kusaidiwa kila kitu na Rwanda” alisema Ndayishimiye, huku akiitaka nchi hiyo jirani kuacha “mara moja kuunga kono waasi.”

Mnamo Desemba 22, 2023, Serikali ya Burundi ilishutumu waasi hao kwa kutekeleza shambulio la silaha dhidi ya raia magharibi mwa Mji Mkuu wa Bujumbura.

Kwa mujibu wa Burundi, takriban watu 20 wakiwemo watoto 12 waliuawa wakati wa shambulizi hilo lililodaiwa kufanua na kundi la waasi la Red-Tabara.

### Mvutano Mpya

Mvutano huu mpya kati ya nchi hizo mbili jirani za Afrika Mashariki unakuja wakati ambapo Burundi inaelekea kwenye uchaguzi wa wabunge, useneta



Rais Ndayishimiye - Picha ya BBC

na serikali za mitaa mwaka 2025.

Uhusiano kati ya Rwanda na Burundi umezorota tangu mwaka 2015 kufuatia mzozo wa kisiasa na kiusalama uliotokana na kugombea muhula wa tatu wa rais wa zamani wa Burundi, Pierre Nkurunziza.

Burundi imekuwa ikiituhumu Rwanda kwa kuwahifadhi na kuwafunza kijeshi wapinzani wake ambao wamekimbilika huko.

Kwa upande wao, Rwanda inaishutumu Burundi kwa kushirikiana na waasi wa vuguvugu la FDLR (Democratic Forces for the Liberation of Rwanda), wanaotuhumiwa kutekeleza mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi (kabila la wachache) mwaka 1994 nchini Rwanda.

Kundi la waasi wa Red-Tabara liliundwa mwaka 2011 na likiwa na takriban wapiganaji elfu moja. Ni kundi la wapiganaji wa Burundi ambalo limekuwa likifanya uasi tangu kuanza kwa mzozo wa kisiasa wa 2015.

Linashutumiwa kwa kuhusika katika mashambulizi kadhaa mabaya na kuvizia nchini Burundi tangu mgogoro uliotokana na changamoto kutaka aliyekuwa rais wan chi hiyo, Pierre Nkurunziza kugombea urais muhula wa tatu mwaka 2015.

Baada ya kuingia madarakani Juni 2020, Rais Ndayishimiye amekuwa akisema mara kwa mara kwamba yuko tayari kufanya mazungumzo na kundi hilo la waasi, lakini limekuwa likigoma na kudai kufanyika kwa uchaguzi upya ambao utakuwa wa kidemokrasia, huru, jumuishi na wa wazi.



## Tangazo

# KITONGA HOUSE OF MILK



“SPORTS LOUNGE”

## Kunywa maziwa ya Kitonga, imarisha afya

Maziwa ya ng'ombe na mbuzi yamethibitika kuwa na mnyumbuliko wa vitamini, protini, mafuta yanayofaa, madini na maji; vitu ambavyo vinahitajika zaidi katika mwili wa binadamu kustawi.

Mazoea ya kunywa maziwa ni nguzo muhimu ya kumsaidia binadamu kuwa na afya bora, kupambana na baadhi ya magonjwa na kumpa kinga inayohitajika katika mwili.

Ni kutokana na ukweli huo, Kitonga Farm imeamua kusogeza karibu huduma ya kusambaza maziwa kwa wananchi.

Sasa maziwa hayo, pamoja na bidhaa zake zingine, yanapatikana Bunju, Barabara ya Mbweni – kama unaelekea Shule ya Moga, Dar es Salaam.

Pia mteja anaweza kufikishiwa maziwa hadi nyumbani endapo anaishi maeneo ya Bunju A, B na Mbweni.

Njoo Kitonga House of Milk kwa kupata maziwa halisi ya ng'ombe na mbuzi kwa kuimarisha afya yako na familia.



Hey!!!  
STOP!  
Let's have  
some Milk!



**Wasiliana nasi kwa namba ya simu: 0748 109 109**  
**Chagua Kitonga Farm, Chagua Afya Njema.**







## Kesi Zilizosisimua

### Ahukumiwa kunyongwa kwa kuua 'hawara' wa mume - V

Hii ni sehemu ya mwisho ya mfululizo wa kesi iliyosisimua zaidi ya mwanamke kumuua mwenzake, kisa; kumtuhumu kuwa hawara wa mumewe. Endelea kumaliza hukumu yake katika sehemu hii ya mwisho.

**M**aelezo hayo yaliendelea kwamba mtuhumiwa alifanya usafi wa kuondoa damu baada ya kuua, ili kuficha ushahidi na kisha alienda kazini na kufanya kazi kama kawada na kisha kurejea nyumbani saa nne usiku. Pia jaji alizungumzia maoni ya mzee wa baraza Mwasabuli Ali.

Kwa mujibu wa maoni yake, Mwasabuli alisema kwamba, haamini kuwa marehemu ambaye alimshitaki mtuhumiwa, anaweza kumuomba mtuhumiwa amwelekeze mahali panapouzwa vinywaji baridi.

Alisema, haamini kwamba marehemu ambaye siyo mgeni hapa jijini Dar es Salaam, asiwe anajua mahali panapouzwa vinywaji baridi.

Mwasabuli alisema pia haamini kwamba marehemu anaweza kumkashifu mtuhumiwa wakati akiwa hapo nyumbani kwa mtuhumiwa.

Mzee huyo wa baraza, alikataa kukubaliana na dhana ya kukasirishwa kwa sababu kama mtuhumiwa alikuwa amekasirishwa kupita kiasi, asingeweza kuuburuza mwili hadi bafuni, kuuchoma moto na baadaye kuzuzika akiwa peke yake, na pia kumwambia house boy wake, "nimemua mbaya wangu."

Pia Mwasabuli alishangaa iweje mtuhumiwa amudu kwenda kazini na kufanya kazi kama kawaida kama vile hakuna kilichotokea. Mzee mwingine wa baraza, Kikoti pia alikubaliana na maelezo ya mwenzie.

Jaji alikubaliana na maelezo hayo ya wazee wa baraza kwamba mauaji hayo yalikuwa hayana maana nyingine isipokuwa dhamira ovu.

Jaji aliendelea kusema kwamba ingawa mtuhumiwa anadai alipatwa na hasira zilizopitiliza, lakini yeye



*Asha Mkwizu*

hakubaliani na utetezi huo kwa sababu ushahidi uliotolewa hapo mahakamani hautoshi kuuamini.

Ili kuweka uwiano, jaji alitolea mfano kesi kati ya Jamhuri dhidi ya Stephano Aloys - ya mwaka 1972 HCD namba 199, jaji aliendelea kusema kwamba, mpaka hapo mashtaka ya kuua kwa kukusudia (Murder) dhidi ya mtuhumiwa yamethibitishwa pasi na shaka yoyote, kama ilivyoainishwa katika kanuni ya adhabu.

Kisha akaendelea kwa kuweleza kwamba anakubaliana na mtazamo wa mazingira, ushahidi wa pande zote mbili na akaendelea;

"Inawezekana haswa, kwa kweli kwamba sheria yetu katika suala la kurukwa na akili (Insanity) limepitwa na wakati na ni la kizamani.

Katika ushahidi wa Dkt. Haule amesema kwamba katika uchunguzi wa kisasa, utofauti kati ya kurukwa na akili na kuondokewa kwa hali ya ubinadamu mkamilifu (diminished responsibility), lipo chini ya mjadala mkubwa kwa sababu halikubaliki.

Bunge kwa hekima yake linaweza

## Kesi Zilizosisimua



## Ahukumiwa kunyongwa kwa kuaa

*Inatoka Uk. 17*

likataka kurekebisha matawi husika ya sheria na kuyaleta ama kuyaongeza katika mstari utakaoenda sambamba na taaluma za kisasa za kitabibu juu ya suala husika.

Na katika nguvu nyingine, kimahakama ikiwemo mojawapo hata ya Afrika Mashariki iwe inafanya hivyo, lakini kama sheria ilivyo, tupo katika mchango wa mawazo kuona mhashimiwa jaji ameelekea katika hitimisho sahihi.”

Katika mahakama ya rufaa ilizingatia rufaa ya kesi ya Agnes Liundi, katika maelezo yake katika kesi hiyo Jaji Bahati alikiri kwamba hayatofautiani sana na kesi kadhaa zilizowahi kufika mbele ya mahakama hiyo.

Aliitaja kesi ya Agnes Liundi, ambaye aliamua kuaa watoto wake kwa kuwapa sumu, baada ya kubaini mienendo isiyofaa kwa mume wake.

Na akaeleza kwamba Agnes alidai mahakamani kwamba yeye aliamua kujiua pamoja na watoto wake ili kwenda “kupumzika” kwa kuwa alichoka kuishi kutokana na madai ya kuteswa na mume wake.

Ilielezwa mahakamani kwamba siku hiyo ya tukio, Agnes alinunua sumu pamoja na juice ya ‘Orange Squash’ na kuchanganya na aliwapa watoto wake wanywe na yeye pia kunywa sumu hiyo.

Katika tukio hilo, watoto watatu walifariki dunia, lakini yeye na mtoto wake mmoja waliokolewa na madaktari.

Katika kesi hiyo mawakili wa utetezi walikuja na hoja ya uwendawazimu (Insanity), wakati mtuhumiwa akitenda kosa hilo, lakini Mahakama Kuu haikuafiki hoja hiyo.

Pia kulikuwa na jaribio la kuleta au kuingiza hoja nyingine ya kupoteza hali ya kibinadamu (diminished responsibility), hoja ambayo pia ilikataliwa na mahakama hiyo.

Jaji Bahati alikataa kuikubali hoja hiyo ya kupoteza hali ya kibinadamu kama

utetezi katika kesi hiyo ya Asha Mkwizu kama ilivyokataliwa katika kesi ya Agnes Liundi.

Kutokana na tafiti za Jaji Bahati, hapakuwa na kipengele chochote cha sheria kinachoeleza juu ya kukasirishwa kupita kiasi.

Baada ya kukataliwa kwa maelezo ya mtuhumiwa yanayohusu kutukanwa, jaji hakuona umuhimu wa kuhusisha vipengele vya sheria ya kanuni ya adhabu na makosa ya jinai vya 201 na 202 kuhusiana na kukasirishwa. Hapakuwa na umuhimu wa kuoanisha hayo.

Katika hitimisho lake la hukumu, jaji alisema; “nimeridhika na tuhuma za mauaji ya kukusudia na zimethibitishwa pasi na shaka yoyote, kwa hiyo basi, mtuhumiwa amepatikana na hatia ya kuaa kwa kukusudia na ninamhukumu kulingana na sheria kama ifuatavyo;

Mahakama: Hukumu iliwasilishwa mbele ya mahakama ikishuhudiwa na mtuhumiwa, wasaidizi wa mahakama na wazee wa baraza, je mtuhumiwa una lolote la kusema?

Mtuhumiwa: Sina la kusema ila nilichosema ni kweli, naiomba mahakama inipunguzie adhabu kwa sababu ya matatizo yote haya, nina mzazi mzee sana na afa yangu ni dhaifu, nimefanyiwa operesheni mbalimbali, ninasumbuliwa na kifobu cha mkojo na uti wa mgongo.

Hukumu: Jaji akaanza kusoma; “Kwa mujibu wa sheria kuna hukumu moja tu kwa makosa ya kuaa kwa kukusudia, nayo ni adhabu ya kunyongwa hadi kifo...

...Alichosema mtuhumiwa katika kesi hii, kinaweza kumsaidia kwa hatua nyingine na siyo kwa mahakama hii. Kwa hiyo basi, nakuhukumu wewe Asha Mkwizu Hauli adhabu ya kifo kwa kunyongwa hadi kufa.”

Tunawashukuru sana wasomaji wetu kwa kuwa nasi hadi mwisho wa kesi hii iliyosisimua. Tunaahidi kuanza mfululizo wa kesi nyingine kwenye toleo lijalo.



## Je, mwisho wa Trump kisiasa umewadia?

Na Peter ANDREA

**M**AJIMBO mawili nchini Marekani; Colorado na Maine, yameondoa jina la Donald Trump katika kinyang'anyiro cha kugombea urais wa nchi hiyo.

Kuenguliwa kwa Trump, rais wa 45 wa Marekani, kwenye majimbo hayo, kunaelezwa na wachambuzi wa siasa kwamba huenda kukaigwa na sehemu zingine, hasa majimbo makubwa, hivyo kuweka kinzigiti kwa kiongozi huyo wa zamani, kurejea Ikulu ya White House, iliyoko Barabara ya Pennsylvania, Washington, DC.

Maafisa wa majimbo hayo mawili, kwa ziadi ya wiki mbili sasa, waliamua kuondoa jina la Trump kwenye mchakato wa kura ya maoni, wakidai wanaitikia nguzo muhimu ya kulinda misingi ya demokrasia na amani ya Marekani.

Trump anatumwa kwa “ukaidi na ukorofi” ambapo anadaiwa kushiriki kwenye vuguvugu la kuvamiwa kwa majengo ya serikali (Capitol Hill) ambamo kuna ofisi kadhaa, ikiwamo mahakama kuu, mabunge na idara zingine nyeti.

Kutokana na ushawishi wa majimbo hayo madogo, inadhaniwa kuwa majimbo mengine kadhaa yanaweza kufuata mkumbo huo, hivyo kumkwamisha Trump kwa mgombea wa urais. Uchaguzi wa Marekani unafanyika baadaye mwaka huu.

Majimbo yanayohofiwa kufuata uamuzi wa Maine na Colorado, ni pamoja na Arizona, Nevada, Oregon, New Mexico, na New York.

Wengi wanaompinga Trump wanasifu mkakati huu wa kisheria kuwa njia sahihi ya kumzuia Trump kugombea. Idai kubwa ya Wamarekani, hasa wasiokuwa wahafidhina, wanamwona kama tishio la uhai wa nchi, bila kumpinga kupitia sanduku la kura.

Wiki mbili zilizopita, Mahakama



ya Juu ya Colorado ilikubali maoni ya mahakama ya chini kwamba Rais Trump mnamo Januari 6, 2021, alishiriki kuhamasisha vurugu za kuvamiwa kwa Capitol Hill, hivyo kumusisha na uasi.

Mahakama ya juu ya jimbo hilo iliamua kwamba, kwa sababu marekebisho ya kumi na nne ya Katiba ya Marekani yanawazuia maafisa wa zamani kupata wadhifa tena ikiwa watakiuka kiapo chao cha ofisi kwa “kuhusika katika uasi.

Baadaya ya jimbo hilo kumuengua Trump, Katiba wa Jimbo la Maine, Shenna Bellows, akitegemea zaidi rekodi katika kesi ya Colorado, aligundua kwamba “ushahidi wa ziada” ulioneshwa kwamba shambulio la Capitol Hill lilikuwa sawa na “uasi.”

Ingawa Bellows alikiri kwamba swali la iwapo Trump binafisi alihusika katika uasi lilikuwa “karibu zaidi,” alihitimisha kwamba uzito wa ushahidi ulithibitisha kwamba “alitumia simulizi ya uongo na udanganyifu kuhusu matokeo ya uchaguzi, hivyo kuwatia hasira wafuasi wake kiasi cha kuwachochea wafuasi wake kufanya uasi wa kuvamia maeneo ya mabunge.

Sehemu ya tatu ya marekebisho ya kumi na nne ya Katiba ya Marekani iliyidhinishwa mwaka 1868, inataka maafisa wa serikali kuzuiwa kupewa ofisi tena ikiwa walikuwa wamesalitii mfumo wa uongozi wa nchi hiyo.

# Mpangilio uwe mzuri ...



*Maktaba Kuu ya Taifa iliyopo Kisutu, Dar es Salaam ilikuwa kwenye ukarabati tangu Julai, 2023, hata hivyo, bado kuna maeneo ndani ya taasisi hiyo yako kwenye mazingira yasiyofaa kwa watumiaji wa huduma zake. Hapa ni moja ya eneo ambalo lilikutwa na Mpigapicha Wetu hivi karibuni.*

*GAZETI hili lilianshwa 2021, kuandaliwa na kusambaswa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaandeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

